

Kama mpangaji, ni muhimu kuwahi kulipa kodi. Ulikubali kufanya hivyo ulipoweka saini kwenye hati ya kukodisha.

Kama umechelewa kulipa kodi, kwa kweli umevunja masharti ya mkataba wa kupangisha na upo nyuma na kodi.

Waweza kuwa na matatizo kulipa kodi, hasa kama kipato chako kinabadilisha au kama ukiumwa.

Ghafla umekosa kulipa kodi halafu upesi umepata tatizo kubwa.

Ukichelewa mno na kodi na huwezi kulipa kiasi cha kupitiliza muda, uangalie.

Ongea na ajenti au kabaila yako mara moja.

Jaribu kukubaliana mpango wa kulipa.

Hii ni mpango kulipa pesa zote unazo ni deni lako—kwa kulipa kidogo kidogo, kwa muda unaofaa.

Utahitaji kulipa pesa za sehemu kuongeza na kodi ya kawaida.

Wewe na kabaila mkubali na mpango – kuhusu kiasi ngapi cha pesa na utazilipa lini.

Kama nyote mkubali uviandikie hivi na nyote weka saini zenu.

### **Je, naweza kuambiwa niondoke?**

Kama kodi yako imechelewa kulipiwa zaidi kuliko siku 14, kabaila anaweza kukupa Termination Notice (Notisi ya Mwisho wa Upangaji) kumaliza mkataba wa upangaji.

Notisi itaeleza una siku 14 kuhama kutoka miliki.

### **Nini itakachotokea kama sihami miliki?**

Kabaila anaweza kuomba kwa Consumer, Trader and Tenancy Tribunal (Mahakama ya Mtumiaji, Mwenye biashara na Upangaji) kumaliza upangaji wako usipohama baada ya notisi ya siku 14.

Hawawezi kukusukuma kuondoka miliki bila agizo kutoka Tribunal.

### **Kuhusu usikilizaji wa kesi kwa Tribunal**

Kwanza utapata barua kutoka Tribunal kukuambia kuhudhuria usikilizaji wa kesi.

Ni muhimu uhudhurie usikilizaji wa kesi kuambia maelezo yako na kuonyesha uthibiti wako.

Ambia Tribunal ukihitaji mkalimani. Mkalimani ni bila malipo.

Katika usikilizaji wa kesi, Tribunal itjaribu kukusaidia na kabaila kukubali mpango wa kumaliza malipo.

Kama wewe na kabaila hamwezi kukubali, Tribunal itaamua na kufanya agizo.

Agizo ni agizo wa kisheria kwa mtu kufanya mambo fulani.

Kufahamu kuhusu kazi ya Tribunal angalia DVD yao kwa YouTube au tembelea tovuti yao.

### **Itakuwaje kama ukihama wakati una deni ya kodi?**

Kama ukihama na bado una deni kubwa zaidi kuliko kiasi cha dhamana, Ajenti au kabaila anaweza kuweka jina lako kwenye

Tenancy Database (Database ya Upangaji).

Kama jina lako lipo kwenye orodha katika database itakuwa vigumu kwako kupanga miliki mingine baadaye.

### **Jinsi gani kuepuka kupata kiporo(deni) cha kodi?**

Kama mpangaji, uwahi kulipa kodi yako. Waweza kupanga kwa njia iliyopanguliwa kulipa kodi yako ili hutachelewa kulipa.

Kwa mfano, pesa za kodi zinaweza kuchukuliwa mara moja kutoka akaunti yako ya benki kwa taraha fulani.

Hakikisha una pesa za kutosha katika akaunti yako ya benki au utalipa ada za benki.

Lazima majenti wakupe chaguo ya njia aina moja ya kulipa bure kama Centrepay, EFTPOS katika ofisi zao.

Kama ukikuwa na shida kulipa kodi wasiliana na Housing NSW (Makazi NSW) ya eneo lako. Labda wataweza kukusaidia.

Pia unaweza kutafuta msaada kutoka mshauri wa fedha kupanga budgeti ili upange hali yako ya fedha.

Kupata maelezo zaidi kuhusu haki na majukumu ya wapangaji, tembelea tovuti ya Fair Trading kwa [www.fairtrading.nsw.gov.au](http://www.fairtrading.nsw.gov.au) au piga simu namba ya 13 32 20.

Kama ukihitaji msaada wa lugha pigia simu 13 14 50.